NAKALA YA MKUFUNZI

Kuelewa na Kuheshimu Hisia za Wengine

KISA CHA 1

Selam alikuwa kwenye mlo wa mchana pamoja na marafiki zake, lakini alipokimbilia msalani aliiacha simu yake mezani. Alipokuwa hayupo, rafiki yake Mwikali aliichukua simu ya Selam na kuanza kuzisoma meseji zake. Ujumbe wa maandishi wa kwanza aliouona ulikuwa ni wa hasira uliotoka kwa mama yake Selam kwa sababu hakufaulu hesabu.

Je, hali hiyo inaweza kumfanya Selam alijisikiaje?

Selam anaweza akahisi kwamba siri yake imeingiliwa na huenda akaacha kumwamini rafiki yake.

Kwa nini Selam asingependa kuwaambia marafiki zake kuhusu matokeo yake mabaya?

Selam anaweza kuyachukulia matokeo yake kama taarifa za siri.

Je, matendo ya Mwikali yanakubalika?

Wanafunzi wanapaswa kuchukulia kanuni zao kuhusu siri inayohusiana na alama za mtihani na simu yao, vilevile yale wanayotarajia kutoka kwa marafiki wao.

Je, marafiki wengine watajisikiaje kuhusu matendo ya Mwikali wakati wa chakula cha mchana?

Wanafunzi wanapaswa kufikiria kile ambacho wangefanya kama wangeona mwenendo usiofaa.

Una maoni gani kuhusu Mwikali? Je, Mwikali alitenda kwa kuzingatia maadili? Je, ungependa kuwa rafiki yake Mwikali?

Majibu yanaweza kutofautiana.

Ungejihisi vipi kama mtu angekutendea hivyo?

Majibu yanaweza kutofautiana.

Je, ni sawa kusoma meseji za wengine? Vipi ikiwa una wasiwasi kuhusu rafiki yako?

Wanafunzi wanapaswa kutafakari kuhusu kanuni zao za siri na mahusiano binafsi na wengine.

Chanzo: *Maudhui haya yanahifadhiwa na Facebook na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.*

Meta | My Digital World

Kuelewa na Kuheshimu Hisia za Wengine

KISA CHA 2

Yonas anaongea na Masese kisha anateleza na kuanguka chini. Masese anafikiri hali hiyo inachekesha sana kisha anampiga picha, lakini Yonas hacheki na anaonekana ameaibika.

Kwa nini huenda Masese akachapisha picha hiyo mtandaoni?

Wanafunzi wanapaswa kutambua nia ya Masese: kupata vicheko au vipendwa kwa kawaida ni nia inayokubalika ya kuchapisha kitu mtandaoni, maadamu kufanya hivyo kusimdhalilishe mtu mwingine.

Kwa nini Yonas ameudhika?

Wanafunzi wanapaswa kutafakari namna ya kuzichukulia hisia za wengine wanapotumia mitandao ya kijamii.

Unafikiri Yonas amwambie nini Masese?

Wanafunzi wanapaswa kuja na mikakati ya kushughulikia tabia hii.

Ungejihisi vipi kama mtu angekupiga picha ya kuaibisha? Je, ungependa iwekwe kwenye mtandao?

Wanafunzi wanapaswa kuchukulia kanuni zao kuhusu kile wanachotaka kisambazwe mtandaoni na wengine.

Je, hali hii ni tukio la uonevu?

Wanafunzi wanapaswa kufikiria jambo linalofanya tendo liitwe uonevu na wajadili mambo mahususi kuhusu hali hii.

Chanzo: *Maudhui haya yanahifadhiwa na Facebook na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.*

Meta | My Digital World

NAKALA YA MKUFUNZI

Kuelewa na Kuheshimu Hisia za Wengine

KISA CHA 3

Victoria ni mwanafunzi mwenye umri wa miaka 15 aliye na ndugu wawili, mama na marafiki wengi anaosoma nao. Victoria na Marek wanasoma wote na wanafanya kazi pamoja kwenye mradi katika darasa la sayansi. Jana, walifanya mtihani wa sayansi na kila mtu alipokea matokeo yake, Marek aligundua kwamba Victoria hakufurahia matokeo hayo. Wiki inayofuata, Victoria hakuja shuleni kwa siku kadhaa, Marek alilazimika kufanya kazi kwenye mradi huo wa sayansi mwenyewe. Aliporudi, Victoria alimwambia Marek kwamba alilazimika kwenda kwa daktari. Hata hivyo, hasemi ni kwa sababu gani.

Je, mtu yeyote anahitaji kujua kuhusu matokeo ya mtihani ya Victoria? Historia yake ya matibabu? Kwa nini?

Wanafunzi wanapaswa kuzichukulia namna ambavyo taarifa tofauti zilivyo na viwango tofauti vya siri. Matokeo ya mtihani ya Victoria ya shuleni ni taarifa nyeti ambazo asingependa marafiki, anaosoma nao au umma kwa ujumla wazijue. Hata hivyo, taarifa hizo siyo za siri kwa wazazi/walezi wake. Pia hali ni hiyo hiyo kwa taarifa za historia ya matibabu, ingawa taarifa hizo ni nyeti sana.

Je, Victoria angependa kuzungumza na nani kuhusu masuala haya?

Huenda Victoria akataka kuzifanya taarifa zake kuwa za siri. Uamuzi huu unapaswa kuheshimiwa. Pia anaweza kuamua kuzisambaza baadhi kwa wengine ila siyo zote taarifa binafsi. Kwa mfano, anaweza kuwaambia hali anayokabiliana nayo katika matokeo yake wazazi/walezi wake, lakini siyo marafiki zake.

Katika maisha yako, ni mifano gani ya taarifa ambazo unataka wazazi/walezi wako wazione lakini siyo marafiki zako au kinyume chake?

Wanafunzi wanapaswa kufikiria machaguo yao wenyewe kuhusu siri.

Chanzo: *Maudhui haya yanahifadhiwa na Facebook na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.*

Meta | My Digital World